

G.J. Measey
P.K. Malonza
and V. Muchai

AMFIBIA

wa milima ya Taita

2009
SANBI
12

ISBN 978-1-919976-49-5

Alama za maelezo

mastakimu	dimbwi
	kidimbwi
	mto
	kijito
	ndani mchangani / chini ya ardhi
mchana / usiku	mchana
	usiku
mwinuko kutoka ufuo wa bahari	nyanda za juu
	nyanda za chini
aina ya mimea	bustani
	msitu
	mgunda

2009
SANBI
Biodiversity Series
12

SANBI Biodiversity Series

Amfibia wa milima ya Taita

na

G.J. Measey, P.K. Malonza na V. Muchai

SOUTH AFRICAN
national
biodiversity
institute
SANBI

2009

2009
SANBI
Biodiversity Series
12

SANBI Biodiversity Series

Halimashauri ya kitaifa ya bioanuwai ya Afrika Kusini (SANBI) iliazishwa tarehe moja Septemba 2004 wakati sheria ya kulinda mazingira: Inayozingatia mazingira (NEMBA) namba kumi ya mwaka 2004 ilipotiwa sahihi na rais Thabo Mbeki. Hii sheria inapanua mamlaka ya kile halimashauri ya kushughulikia mimea kuhusisha jukumu la kuangalia wanyama na mimea ya Afrika Kusini na inahushisha mipango ambayo inatambuliwa kwa kulinda, kutafiti, kuelimisha na huduma za wangeni iliyotayalishwa na halimashauri ya kushughulikia mimea na mashilika tangulizi katika karne iliyopita.

Maono ya SANBI ni: Wingi wa bioanuwai kwa kila mwenyeji wa Afrika Kusini.

Mwongozo wa SANBI ni kupigania utafiti, utunzi, matumizi mwafaka, kuangalia na kufurahiwa kwa mseto wa bionauwai kwa watu wote.

Mfululizo wa Bioanuwai wa SANBI huchapisha ripoti za utafiti, technologia, kongamano na mambo na miradi mingine inayoanzishwa na au inayotekelezwa kwa ushilikiano na SANBI.

Mhariri wa kiufundi:	Gerrit Germishuizen
Mtindo na mpangilio:	Elizma Fouché
Mtindo wa jalanda	Elizma Fouché

Kitabu hiki kunukuliwe kama ifuatavyo
MEASEY, G.J., MALONZA, P.K. & MUCHAI, V. 2009. Amphibians of the Taita Hills / Amfibia wa milima ya Taita. *SANBI Biodiversity Series* 12. South African National Biodiversity Institute, Pretoria.

ISBN 978-1-919976-49-5

© Published by: South African National Biodiversity Institute
Obtainable from: SANBI Bookshop, Private Bag X101, Pretoria, 0001 South Africa.
Tel.: +27 12 843-5000. E-mail: bookshop@sanbi.org. Website: www.sanbi.org.
Printed by Seriti Printing (Pty) Ltd, P.O. Box 24829, Gezina, 0031 Pretoria.

Yaliyomo

Utangulizi iv
Maelezo v
Shukrani vi
Bioanuwai 1
Hali ya anga Taita 4
Amfibia 8
  Kuangua 8
  Makwapa 8
  Kuangua moja kwa moja 11

Xenopus borealis	kichula machi	12
Hemisus marmoratus	kichula nguwe	16
Callulina dawida	kingo'mbe	20
Arthroleptis xenodactyloides	kichula magala	24
Amietophrynus gutturalis	kiwandu	28
Mertensophryne taitana	kiwandu kitini	32
Leptopelis concolor	kichula mudi	36
Ptychadena mascareniensis	kingele	38
Ptychadena anchietae	kidadu	42
Phrynobatrachus scheffleri	magala machi	46
Amietia angolensis	kichula moda	48
Hyperolius glandicolor	kibarangela	50
Kassina senegalensis	kimori	54
Chiromantis petersii	kichula ifuwa	56
Boulengerula taitana	kilima mdawida	60
Boulengerula niedeni	kilimamrota	64

Marejeleo zaidi 69
Vikundi na mashirika 70
Kuhusu waandishi 71
Kielezo 74

Utangulizi

Kitabu hiki ni nakara ya amfibia wanao patikana katika Milima ya Taita. Amfibia ni baadhi ya wanyama wasiojulikana sana na pia hawavutii kwa sababu ya miili yao inateleza. Wao pia ni baadhi ya wanyama wanaokabiliwa na tishio la kunangamia kutokana na mwingilio na wa binadamu. Kitabu kitasaidia kuwafahamu amfibia na umuhimu wa kuwalinda. Ni matarajio yangu kuwa hiki kitabu kitawasaidia wasomaji kuanza kuwatambua amfibia na umuhimu wa kuyalinda mazingira yao na haswa misitu ya kiasili ambayo inategemewa na wengi wa viumbe hawa. Natumai kuwa utapata kujivunia (kama ninavyo) kwa kufahamu kuwa wanyama hawa hupatikana tu Taita na sio mahala pengine ULIMWENGUNI KOTE.

Tunaishi mahali penye utajiri mwingi na pa kuvutia ambapo pengine palikuwa pazuri zaidi kabla hatuja ukata msitu wa kiasiri. Kulingana na wanasayansi Milima ya Taita imepoteza zaidi ya asilimia tisaini na nane ya musitu katika kipindi cha miaka 200 iliyopita. Ni wajibu wetu kuona kuwa hakuna uharabifu mwingine unaotokea lakini tujaribu kurejeshe umaridadi wa hii sehemu kadri tunavyo weza. Hii pia itakuwa ni faida kwetu kwa njia kadhaa kama kupata maji zaidi, kuimalika kwa mavuno ya chakula na pia kulinda uhaiwai huu tunao wa kipekee.

Bidii na kujitolea kwa waandishi kumezaa matunda ya kazi iliyo kamilika na kwa hakika itakuwa ya manufaa kwa wasomaji.

James Mwang'ombe
Project Coordinator
The East African Wild Life Society
10 October 2008

Maelezo







Kalenda hii inaonyesha mabandiliko ya mwezi kwa mwezi ya mvua na joto kwa vivuli vya samawati na nyekundu. Mishoro ifuatayo inaonyesha wakati kiume wanaita, wakati mayai na viluwiluwi wanapatikana, na mwisho wakati chura wazima upatikana

Urefu wa wastani wa kiume na kike imepewana kwa kulinganisha na kiasi cha mkono wa kawaida. Chura mnaowapata waweza kuwa wadogo ama wakubwa kuliko kiasi cha wastani

Ramani hii inaonyesha sehemu ambazo tumewapata aina hizi za amfibia. Inawezekana kuwapata sehemu zingine na tunawapa changamoto muwatafute!

Shukrani

Tunashukuru shirika la "Critical Ecosystem Partnership Fund" kwa uchapishaji wa hiki kielezo.

CRITICAL ECOSYSTEM
PARTNERSHIP FUND

Kimetafsiriwa toka kingereza hadi kiswahili na Ahmed Omar (Makavazi ya kitaifa ya Kenya).
Tunamsukuru sana Muthama Muasya (Chuo kikuu cha Cape Town) kwa usaidizi wake kwenye sehema ya swahili

Mwenye picha: Picha zote zime tolewa na mwandishi wa kwanza isipokuwa:

Ukurasa 3:	Mwangi Githuru:	*Turdus helleri*
Ukurasa 8:	César Barrio:	*Salamandra algira*
Ukurasa 23:	Anthony Herrel:	*Callulina dawida* alama
Ukurasa 49:	Alan Channing:	*Amietia angolensis*
Ukurasa 54:	Alan Channing:	*Kassina senegalensis*
Ukurasa 71:	Krystal Tolley:	Homo sapiens JM

Bioanuwai

Bioanuwai ni tamko linalo onyesha tarakimu za aina ya viumbe walio katika sehemu fulani. Katika sehemu za nchi zilizoendelea tarakimu za viumbe hujulikana kwa maana wanabiologia wamekuwa wakifanya utafiti kwa muda ilihali sehemu zingine hazijafanyiwa utafiti wa kutosha na huwa na bioanuwai isiyojulikana kiwango chake. Katika mwaka wa 1999 wanasayansi walichunguza mielekeo ya bioanuwai duniani na kuamua kuwa eneo zingine ni spesheli na zina idadi kubwa ya viumbe kwenye sehemu kidogo. Haya maeneo yanajulikana kama 'Maeneo makuu ya Bionanuwai'. Kati ya maeneo makuu 12 ya bioanuwai yaliyotabuliwa moja linaitwa 'Ukanda wa milima ya mashariki na misitu ya pwani' katika Afrika Mashariki.

Eneo la ukanda wa milima ya mashariki linaanzia kule Udzungwa huko mbali Kusini mwa Tanzania mpaka Milima ya Taita, Kusini mwa Kenya. Milima katika hii sehemu ina umri mmoja (karibu miaka milioni mia mbili) na imekuwa ikitega mvua inayotoka Bahari Hindi. Hii inamaanisha kuwa hii milima imeweka joto na hali ya unyevu ambao huhitajika ili kutunza misitu ya kiasri mamilioni ya miaka kabla ya wanadamu kuishi katika sehemu hii. Katika kipindi hiki kirefu hali ya anga haikuwa imara kwa ajiri ya kupitia misimu mingi ya unyevunyevu na kiangazi, kila moja ikidumu miaka elfu nyingi. Matokeo yake ikawa ya kwamba sehemu za chini za milima zilifanyika misitu (wakati wa mvua) na tena kufanyika nyika (wakati wa kiangazi). Milima ya Ukanda wa Mashariki ilikaa msitu kwa muda huu wote, kwa hivyo misitu ikawa inashikana wakati wa mvua na kutengana wakati wa kiangazi. Hii ilipea nafasi wanyama na mimea inayoishi katika misitu kutembea na kuenea kati ya milima na kutengana wakati wa kiangazi. Ebu fikiria kama lile eneo lote lilikuwa na sasa hawa wanyama wote wanasukumwa katika sehemu za misitu juu ya milima!

Saa hii, tunaishi wakati wa kiangazi ulimwenguni na nyika huwa kizingiti cha wanyama na mimea wote wa msitu kutoweza kutembea kati ya milima ya Ukanda wa Mashariki. Inaaminika kuwa mabadiliko mengi ya kuungana na kuachana kwa Milima ya Ukanda wa Mashariki ilichangia kuwepo kwa idadi kubwa ya aina ya viumbe wanaopatika katika eneo hili maalum la bioanuwai. Wakati huu (na wakati wa kiangazi hapo mbeleni), Milima ya Ukanda wa Mashariki imekuwa hifadhi ya

Sehemu zilizokuwa zimefunikwa na misitu sasa ni tupu na zina vijisehemu tu kidogo zenye miti ya kingeni.

Sehemu za chini katikati mwa milima ya ukanda wa mashariki, mvua ni ya kiwango cha chini.

maelfu yawanyama na mimea wa aina tofauti ambao hawawezi kuishi nyikani. Hii milima ni kama visiwa vinavyozungukwa na bahari ya nyika. Kwa vile aina tofauti za wanyama na mimea wametengwa kwa maelfu ya miaka, hawa viumbe wamekuwa spesheli na wengi hupatikana kwenyesehemu za juu za kila mlima. Milima ya Ukanda wa Mashariki ina viumbe wengine ambao hawapatikani mahali pengine ulimwenguni na kati ya wanyama wote wenye uti wa mgongo ni amfibia ambao ni wengi, pengine ndio wengi kabisa Afrika.



Baadhi wanyama wapatikanao Taita peke yake. a, Taita-chanua (*Impatiens taitana*); b, Taita kinyonga (*Kinyongia boehmei*); c, Taita ndege (*Turdus helleri*); na d, Taita kipopo (*Cymothoe teita*).

Isiwe ya kustaajabisha kuwa Milima ya Taita iko na wanyama na mimea wengi wasiopatikana mahali pengine duniani. Hawa ni pamoja na ndege, mmea maua, vipepeo, na wengine. Hiki kitabu ni kuhusu amfibia wa Milima ya Taita hata kama wanapatika mahali pengine pia lakini tutashughulikia wale wapatikanao hapa peke yake. Tutaangazia pia mahali wanaishi na jinsi tunaweza kuwatambua. Ni matarajio yetu kuwa unapofahamu vile wanavyokaa utasaidia katika kuwalinda na kuwatunza hawa wanyama wa ajabu na spesheli.



Milima ya Taita iko kusini-mashariki mwa Kenya, kilomita 160 kaskazini-magharibi mwa bahari hindi.

Hali ya anga Taita

Sehemu yote ya Afrika Mashariki hupata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Mvua ya Masika ambayo ndiyo nyingi ni kutoka mwezi Machi hadi Mei na pia mvua kiasi 'Vuli' kutoka Oktoba hadi Desemba. Wakati wa msimu wa kiangazi, mvua kidogo huwa inanyesha mara kwa mara na kwa hivyo hakuna mwezi ambao hakuna mvua. Kado na mvua, kuna kipindi kimoja cha baridi (Julai) na Februari ndiyo mwezi ambao kuna joto jingi zaidi.

Mvua

Sehemu kadha za Taita hupata mvua na zingine huwa zimekauka. Kwa ujumla, sehemu zilizo inuka huwa na unyevu kwa kuwa zina uwezo wa kutega mawingu ya mvua yanayopita (Kwa mfano Mghange na Vuria). Lakini sehemu zingine ziko katika upande wa pili wa mlima ambao huchukua mvua yote kutoka kwa mawingu. Mvua hutoka kwa Bahari Hindi iliopo kusini mashariki, kwa hivyo sehemu zilizoko kaskazini magharibi mwa Taita na nyuma ya milima hupata mvua iliyopungua. Mfano ni sehemu ya Irizi ambayo ni kavu ingawa iko sawa na Wundanyi kutoka ufuo wa bahari na hupata mvua zaidi. Irizi iko upande wa kivuli cha mvua mwa Ngangao ambayo huchukua asilimia kubwa ya mvua kabla ifike Irizi.

Miaka tofauti pia iko na viwango tafauti vya mvua na inaweza adamana na ngurumo za radi wakati wa kiangazi. Mfano mzuri ni mwaka 2007 wakati mvua isiyo kwa msimu iliyofikia kiwango cha 100 mm



Tarakimu za mvua na joto huko Mwachora mwaka 2006 (ilinakiliwa na Oliver Mwakio). Mlima Mwachora huko juu kidogo (mita 1 630 kutoka ufuo wa bahari) na hupata mvua nyingi.

Katika kivuli cha mvua. Ingawa sehemu hii iko mita 1 400 kutoka ufuo wa bahari bado ni kavu na miti na amfibia wachache pia.

ilinyesha katika sehemu nyingi za Taita. Nyakati za kiangazi hupata mawingu ambayo huleta mvuke kwa sehemu zilizoinuka. Misitu ya kiasili huwa na faida ya kutega huu mvuke ambao hutiririka mpaka kwa mizizi. Hii inamaanisha katika misitu ya kiasili mchanga huwa na unyevu na mito inakuwa na maji kwa mwaka wote ikitimiza mahitaji ya maji kwa watu wanaozunguka msitu. Mashamba ya eucalyptus ni



Tarakima za mvua na joto kutoka Chawia katika mwaka 2007 (imenukuliwa na Christopher Ngeti). Chawia iko na mita 1 604 kutoka ufuo wa bahari na ina urefu karibu na Mwachora lakini hupokea mvua kidogo kwa sababu iko nyuma ya Mlima Iyale.



Tarakimu za joto kutoka Jora (600 m kutoka ufuo wa bahari), Piringa (1 000 m) Sagalla (1 200 m), Mbololo (1 320 m), Mwachora (1 630 m), na Ngangao(1 650 m) mwaka wa 2006. Kadri sehemu ilivyo juu ndivyo joto inavyo pungua lakini sehemu zote zina hali sawa ikiwa na vipimo vya juu mwezi wa Februari na vipimo vya chini zaidi mwezi wa Julai.



Tarakimu za joto kutoka (a) msitu wa Ngangao na (b) shamba moja Wundanyi katika siku 15 za kwanza za mwezi Mei 2006. Utaona vile joto ya hewa (samawati) inabadilika sana ili hali joto mchangani (kijani kibichi) haibadiliki sana, ili hali chini ya ardhi kabisa (hudhurungi) joto haibadiliki. Hali ya joto msituni hukingwa kutokana na mabadiliko na miti ili hali joto hewani huko kwa mashamaba hupanda na kushuka.

Utaona kwamba tarehe tisa Mei kulikuwa na mawingu (na mvua nyingi) lakini tarehe 10, 11, na 12 Mei kulikuwa na jua na joto.

mbaya kwa sababu hunyonya na huelekeza maji ndani ya ardhi. Vijito vilivyokuwa vikitiririka katika sehemu zingine vilikauka baada ya eucalyptus kupandwa. Hali hii hasa iko mbaya kwa eneo la Sagalla hivi kwamba maji hayawezi kuchimbwa chini ya ardhi wakati wa kiangazi.

Joto

Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya joto na mwinuko kutoka ufuo wa bahari hivi kwamba sehemu zilizo na joto zaidi ziko chini na zile ziko juu kwa milima ni baridi zaidi.Vipimo vya joto hubadilika kulingana na uwepo wa mawingu (baridi nyingi mchana na joto usiku) au hamna mawingu (joto jingi mchana na baridi usiku). Hali hii pia hubadilika kulingana na mimea iliopo. Mtu akitembea kwa msitu huhisi baridi lakini usiku huwa na joto zaidi kuliko mashamba kwa vile hutega joto ya machana.

Kuna tofauti kubwa baina ya viwango vya kila siku kati ya mahali tunapoishi na mashamba yetu na ardhi chini ya miguu yetu. Kama vile ungetarajia viwango vya joto kwenye chini ya ardhi huwa havibadiliki, na unapotokea juu ya ardhi ni dhahiri kwamba waweza kupata tofauti kila siku. Kuna tofauti pia baina ya shamba na msitu. Uwepo wa kivuli cha msitu hufanya hewa kuwa baridi hata wakati wa joto. Wakati wa usiku, hewa iliyoko ndani ya msitu haibadiriki na kuwa baridi kama ya nje hivyo basi msitu huhisi joto.

Amfibia hupata joto ya mwili kutoka kwa mazingira yaliyo yazunguka, kama ilivyo reptilia na wanyama wasio na uti wa mgongo. Hii inatokana na jina ‘ectotherm’ likimaanisha nje (ecto) na joto (therm). Amfibia huhitaji mazingira yaliyo na joto na unyevu hivyo basi wingi wa mvua na joto huku milima ya Taita ni mzuri kwao. Hakika mastakimu yale wanapopatikana huwa na tofauti kubwa baina ya joto na unyevunyevu. Misitu ya kiasili ni sehemu zilizo na vipimo vya joto visivyo badilika na huwa nyevu. Viwango vya joto kwenye mashamba yaweza kubadirika na kuwa kavu sana ama kuloa. Hivyo basi jamii tofauti za amfibia hupatikana kwenye misitu na mashamba, ili hali wengine hupatikana sehemu zote mbili.

Mvua unyesha ndani ya msitu kali ambapo joto iko imara.

Amfibia

Amfibia ni viumbe wenye uti wa mgongo walio na ngozi spesheli yenye unyevu na ambayo wanatumia kupata hewa ya oksijeni na pia kuwa na mapafu mawili kama wanadamu. Wao hutaga mayai ambayo yana ute mzito na hayana kauri ngumu. Hii inamaanisha amfibia hushirikishwa na maji.

Duniani kuna aina tatu wa amfibia wanaojulikana kama chura, salamanda na cicilia. Afrika chini mwa Sahara kunapatikana tu chura na cicilia na wote hupatikana kwenye milima ya Taita.

Kuangua

Shuleni huwa tunafundishwa juu ya maisha ya amfibia ikiwa: mayai ambayo yana ute mzito hutagwa kwa maji na huangulia na kuwa viluwiluwi. Hivi viluwiluwi huwa wakubwa, hupata miguu na mwishowe mkia hupungua na miguu kuwa mikubwa na kuwa kichura ambaye hugeuka na kuwa chura mkubwa.

Makwapa

Kwa chura wengi, dume hushika kike kwa kiuno ama nyuma ya miguu ya mbele kabla ya kutaga mayai na utungisho. Hawa chura walioshikamana husemekana wako kwa makwapa (Kilatini ikimaanisha kukumabtia) kwa kiuno au makwapa matawalia. Hii sio ngono kwa sababu



Picha ikionyesha mifano ya amfibia tofaouti – a, cicilia; b, chura; c, salamanda.



Michoro na picha kuonyesha viwango tofauti vya kukua kwa chura – a, mayai; b, viluwiluwi wadogo; c, chura waliokomaa wakiwa kwa makwapa; d, chura mdogo mwenye mkia; e, chura wakiwa kwa ngono.

mayai hayatungwi hadi wanyama waende kwenye mahali pa kutagia mayai, na mutindo wa kushikamana unaweza badilika ili wao wafanye hivi. Pia sio kila chura wa kiume akishika kike lazima atunge mayai yake kwa sababu wa kike wanaweza kuwakataa, au dume zingine zinawazindi nguvu na kuwatoa kwa makwapa.

Kwenye milima ya Taita sio vingumu kuona mpangilio huu wa maisha ya chura. Hebu jaribu kuangalia katika kindibwi ama shimo lenye maji wakati wa mvua, kwanzia Juni hadi Septemba haya maji hukauka ikimaanisha hawa chura huwa na muda mfupi wa kuzaana unaoambatana na msimu wa mvua.

Chura wa kiume hupiga kelele kufahamisha wale wa kike mahali walipo na kila aina ya chura huwa na mlio wa kipekee. Watu wengi wanajua hizi sauti hata kama saa zingine hawajui kama ni chura wanotoa hizi sauti! Wakati mvua inapoanza (Oktoba na Novemba) hizi sauti ni nyingi na hutoka mahali popote ambapo maji yanakusanyika. Aina zingine za chura huzaana huu wakati peke yake, ili hali wengine huendelea na kutoa hizi sauti na kuzaana wakati wa msimu wa mvua mfupi na ule mrefu.

Chura wa kike huvutiwa na kelele za chura wa kiume na wanauwezo wa kuchagua kutoka chura mmoja kutokana na sauti yake. Akisha

Churamiti wa kiume akiitana.

chaguliwa chura wa kiume (mara nyingi mdogo) humpanda chura wa kike na wao huenda kutaga mayai. Wengine huweka mayai moja kwa moja kwa maji kwa vijikamba, mikusanyo ama kama mikeka inayoelea. Wengine hutaga mayai juu ya majani nje kidogo ya maji ili viluwiluwi wanapoanguliwa waweze kuanguka majini na kuanza kuongelea.

Viluwiluwi hula chakula tofauti na chura wakubwa. Wengi wao hula aina ya mimea midogo ya kijani kibichi ambao hukua kwa wingi kwa maji yasiyo na chumvi, ambayo hupa maji rangi ya kijani ama kupaka vitu vilivyo majini ute wa kijani. Viluwiluwi hula hiki chakula na meno spesheli. Kila aina ya chura huwa na meno aina yake yanayoweza

Mayai ya cicilia wa Taita yakionyesha kiinitete kikikua kuzunguka kiiniyai.

kutumika kumtabua kiluwiluwi gani anakuwa chura aina gani.

Kuangua moja kwa moja

Sio amfibia wote ambao huwa na viluwiluwi. Aina kadhaa wa chura wa Taita hawatagi mayai majini bali kwa majani yaliyokauka katika misitu au dani ya udongo wenye unyevu. Hawa chura huwa wana faida ya kuwa hawahitaji kuingia kwa maji kuzaana. Hawahitaji kungojea mpaka mvua ndio watage mayai. Hii hali ya kuwa huru na maji inamaanisha wanaweza kuwa mahali popote mara nyingi bali na maji. Mayai yao huwa na ute mzito unaoyazingira kama ilivyoelezwa hapo mbeleni na hii inamaanisha kuwa yanaweza kukauka kwa hivyo lazima chura watafute mahali penye unyevu ili watage mayai. Chura hawa na cicilia ndiyo chura wa ajabu kwa milima ya Taita (tazama ukurasa 3). Hawa ni pamoja na wengine ambao hawapatikani kwingine duniani na maisha yao haikuwa inajulikana kabla ya utafiti wetu. Tunataraji utafurahia kusoma hiki kitabu kuwahusu hawa chura kama tulivyo furahia kutafiti juu ya maisha yao yanaosisimua.

Xenopus borealis







Nje ya maji hukaa chura wa kutisha atembeaye kwa ungumu. Ona miisho ya rangi nyeusi kwa makucha ya miguu.

kichula machi



Huyu chura anatokezea juu ya maji yenye matope. Tazama mishono kwa upande kwa mwili na karibu na macho.

Chura wengi wana uwezo wa kutembea nchi kavu na pia kwa maji, na wanaweza kuruka au kutembea haraka kukwepa kushikwa. Chura wenye makucha si wepesi kwa kutembea nchi kavu lakini wao huonekana wakati wa mvua kubwa kwenye nchi kavu wakitemeba huku na huko. Chura hawa pia hupatikana wakitembea kwenye nchi kavu baada ya vidimbwi kukauka ambapo hutafuta makaazi mahala pengine. Ingawaje si wepesi kwa kutembea, wao ni waogeleagi mahiri. Ni rahisi kuwaona wakati wa usiku kwenye vidimbwi na mitaro ya maji hasa ukiwamulikwa na tochi. Ukiwashtua wao hujificha matopeni. Wakati mwingine huonekana wakielea juu ya maji na wakati mwingine hula wadudu wa maji na huruka nje ya maji kuwashika wadudu wanapopita karibu.

Ni vigumu kumkanganya huyu chura na vyura wengine wa Taita. Miguu ya nyuma ni mikumbwa na ina matuta yaliyo na makucha meusi ya mwisho wa vidole vinne vya kwanza

Xenopus borealis (kuendelea)



Hawa chura huwa wanakaa kwa maji usiku na vidole vyake vikiwa vimenyooshwa kuhisi mienendo wa kitoeo.

(hivyo kaitwa chura wa makucha). Wao huonekana wamefunikwa na mishono ambayo ni viungo vya kuhisi mazingira yake majini. Wao hutumia viungo hivi kutambua chakula kiliko majini, hii ikiwa ni wadudu, samaki, na viluwiluwi hata vyake pia. Chura hawa wana ngozi nyororo na telezi hivyo basi ni vigumu kuwashika mkononi na hukwaruza sana kwa makucha yao.

Wakati wa mvua kubwa waweza kuwasikia, chura wa kiume huita kwa sauti ya 'brrrrr brrrrr brrrr'

Viluwiluwi wa huyu kiumbe hufanana na samaki wadogo.

ambayo husikika wakati unapokaribia maji. chura wa kiume hukumabatia wa kike katika sehemu zao za manena wawili huogelea wakiwa pamoja wakizunguka kindibwi ilihali wakiweka mayai yao moja moja kwa majani na mawe kubwa ama ndogo. Vuluwiluwi wake hawafanani na wa chura wengine Taita juu huwa wazi na huning'inia kwa maji na mikia yao ikitikishwa kutoka upande mmoja hadi mwingine kwa maji na huchuja chakula kutoka kwa maji. Videvu viwili vikubwa huonekana kwa pembe za mdomo na hufanana na ngogo lakini humea miguu hivyo kujulikana ni chura.



Sehemu ya tumboni ya chura gando wa kaskazini ina madoadoa ya hudhurungi miguuni na mikononi.

Aina hii ya chura hupatikana kwa maeneo ya juu Kenya, Tanzania na pengine Uganda.

Maelezo ya pembeni

Hemisus marmoratus







Huyu chura huwa na mapua koda na rangi ya marumaru.

kichula nguwe



Jike ni mkubwa kuliko dume anaye jichimbia mikono yake kwa upande na kuchukua hii nafasi wakati wa makwapa.

Ni vingumu kukanganya aina hii ya chura kwa wengine wanaopatikana Taita. Yeye hutumia kichwa chake kidogo kinachofanana na cha nguruwe kuchimba mchangani au kwa udongo wakati wa mvua karibu na mito ambapo hukaa mchana. Huyu chura huchimbwa mara kwa mara wakati mashamba yanalimwa. Usiku, hasa wakati wa mvua wao hutokea na kutembea kwa mashamba wakila wadudu ambao huwashika kwa kuwalenga na ulimi mwenye nguluu. Katika sehemu zingine kama mabonde ya Mwatate na Sagalla hawa vyura ni wengi lakini kwenye sehemu zilizojuu za Taita ni nadra kuwaona.

Hawa chura wana mdomo ambao hutoa ulimi kama risasi (tofauti na chura wengine ambao huchukua

Hemisus marmoratus (kuendelea)

chakula kama kulamba). Ulimi umegawanywa sehemu mbili ambazo huzunguka mchwa ama siafu punde inapoingusa. Huyu chura ana uwezo wa kubadili shabaha kadri mchwa na siafu wanavyotembea haraka. Mapua yake ni madogo, na hawa chura hawawezi kula wadudu wakubwa na kwa hivyo wana uzoefu wa kula mchwa na siafu.

Hawa chura husikika wakati wa misimu yote mbili ya mvua wale wa kiume wa kituoa sauti 'quwark', katika sehemu zilizo karibu na mahali wanapozaliana. Miguu ya hawa chura ni mifupi kwa hivyo wao hujishikilia katika upande wa chura wa kike. Pamoja hutaga mayai kwa kikundi kwa shimo kwa maji yaliyosimama. Viluwiluwi huwa na pezi kubwa ya mkia.



Chura pua nguruwe upatikana wakitembea kwenye sehemu zenye mchanga wa changarawe baada ya mvua kubwa

Aina hii ya chura hupatikana kama sehemu kubwa nje ya Milima ya Taita, kuanzi Afrika Kusini mpaka Misri na Afrika Magharibi.

kichula nguwe

Maelezo ya pembeni

Callulina dawida







Huyu chura hutembea polepole kwa majani yaliyokauka na ndio jina la kiasri 'King'ombe'.

kingo'mbe

Inakabiliwa na tisho kubwa la kuangamia Hupatikana Taita pekee.



Wanyama wengi wana macho yenye rangi samawati inayong'aa, na mtindo wa ngozi inaweza kuwa hudhurungi/majano ikifanana na majani yaliyokauka kwa msitu.

Ingawa tunajua chura wanaruka, huyu chura huwa anatembea kama ng'ombe juu ya matawi yaliyokauka katika misitu wa kiasili ya Dawida na Mbololo. Wana miguu mifupi na vidole virefu vinavyostahimili ya kupanda miti midogo na mimea inayotambaa. Wakati wa mchana hujificha kwa majani yaliyokauka lakini usiku wao hupanda miti midogo kwa msitu ambapo vyura wa kiume huita kwa sauti yenye milio mitatu 'kru kru krru' Ana ngozi sugu inayotoa maji maji ambayo yana ngruu anaposhikwa. Wanapotishwa hujufurisha mwili kuonekana wakubwa.

Aina hii ya chura hupatikana katika misitu ya kiasili ya Taita. Kwa sababu makaazi yao ni haba na idadi yao ni dogo na iliyotapakaa, huyu chura anatambuliwa kama anayekabiliwa na tisho kubwa la kuangamia. Hii inamaanisha ya kwamba hatua mwafaka zahitajika kuzuia huyu chura kuangamia. Wao hupatikana kwenye mashamba machache yenye

Callulina dawida (kuendelea)



Chura ambaye ameangua ni mdogo akikalia kidole.

miti ya kiasili na hizi sehemu ni za maana ili hawa vyura waweze kutembea kutoka kipande kimoja cha msitu hadi kingine. Kwa kuweka na kulinda vipande hivi vya misitu midogo unaweza kusaidia kulinda hivi chura dhidi ya kuangamia.

Utafiti wetu katika misitu ya Taita umedhihirisha tabia za uzazi zisizo za kawaida. Karibu mayai 40 hutagwa katika tawi kubwa kati ya matawi yaliyo kauka katika misitu ya kiasili kati ya mwezi Agosti na Septemba wakati wa kiangazi. Huyu chura huangua moja kwa moja (ukurasa 10) na kwa hivyo hawana hatua ya viluwiluwi. Chura jike huyalalia haya mayai kuwalinda kutokana na maadui kama wadudu na ndege ambao huwala mayai. Kati ya yale mayai arobaini ni machache pekee ambayo huangua na yale mengine hutengeza mfano wa kiota chenye mvuke kwa yale mayai yatakayo angua ili yasikauke.

Chura jike huyakalia mayai kwa muda wa miezi tatu mpaka yawe karibu kuangua vyura wadogo. Kukaribia mwisho wa kipindi hiki, wakati mvua inaanza kunyesha, chura jike huyala haya mayai tasa, akihakikisha kuwa ako na nguvu ya kutosha kwa kipindi kile anayalalia mayai. Wale chura wadogo wanaoangua (wenye urefu kama milimita 10) katika mwanzo

Alama spesheli inaonekana kana kisaduku cha rangi ya machungwa chini ya ngozi ya chura.

wa Desemba hukua haraka kufikia ukubwa mara mbili katika kipindi cha miezi minne, kwa kula wadudu wadogo kwa majani yaliyokauka. Wanaweza pia kupanda kwa haraka kuepuka maadui wanaowala kama siafu. Baada ya mwaka mwingine wao huwa wamekua karibu kufikia kiwango cha chura amabao wanaweza zaana kwa mara ya kwanza.

Kuna mambo mengi zaidi ambayo tunahitaji kuyafahamu kuhusu aina hii ya chura ili kuweza kuchangia katika utunzi wake. Zaidi ya vyura mia moja wamewekwa alama na vifaa spesheli (anagalia picha inayofuata) kwenye sehemu za ndani za paja. Ukimuona chura mwenye hii alama tafadhali mjulishe James Mwang'ombe katika Shirika la wanyama pori la Afrika Mashariki.

Hawa chura huonekana milima ya Taita pekee nasio mahali pengine duniani kwenye ofisi ya Wundanyi.

Maelezo ya pembeni

Arthroleptis xenodactyloides







Jike (a) ni wakubwa kuliko dume (b) na huwa wamefura na mayai na huonekana wanono.

kichula magala



Urefu wa chura walionanguliwa ni nusu ya wale wazima, ingawa wazima ni wadogo. Wengi wa chura hawa wana ule mfano wa shisha kwenye mgongo.

Huyu chura ni mashuhuri sana Taita na anaweza patikana kwa msitu wowote ama kwa mashamba. Yeye huishi kwa majani yaliyokauka ambapo hula wadudu wadogo kati ya majani. Wao ni wadogo sana wale wa kike wakifikia ukubwa wa milimita ishirini na tatu na wa kiume kumi na saba pekee ikiwa ni ukubwa wa kidole chako cha gumba. Wana rangi moja na majani yaliyokauka toka hudhurungi hadi nyeusi, haswa wakiwa na mfano wa shisha kwa mgongo. Mwito wa chura wa kiume ni mdogo sana unaofanana na mlio wa chenene ambao unawezasikika ukitoka kwa msitu mwaka mzima, hasa baada ya mvua. Wanapatikana katika vipande tofauti vya msitu na kwa hivyo hupatikana kwa urahisi wakati unatembea kuwaelekea na kuwatazama chini ya miguu yako. Wao ni wakubwa tu kidogo kama chenene na wakiruka hutweka kwa majani.

Wakati wa makwapa, chura wa kiume hujishikilia kwa migongo ya kike na wawili huweka mayai kama 25 katika majani yaliyo kauka. Waume hukaa katika ile sehemu ilikulinda mayai. Huyu chura huangua mayai yake moja kwa moja na kuwa chura

Arthroleptis xenodactyloides (kuendelea)

(ukurasa 10) na kwa hivyo baada ya siku 30 wao huangua na kuwa vyura wadogo, wenye urefu wa milimita tano. Wao hukua na kuwa vyura wazima chini ya muda wa miezi sita.

Utafiti wa kijenetiki unaonyesha kuwa hawa chura huwa wanabebwa na maji wakati wa mvua na wale waliokomaa hubebwa kilomita nyingi toka msitu mmoja hadi mwingine. Kwa mfano chura ambao walishikwa msitu wa Ngangao walipatikana wakiwa na uhusiano wa karibu na wale wa Mbololo.

Kado na Taita hawa chura hupatikana katika sehemu kubwa ya mashariki, kusini na katikati mwa Afrika.

Chura mbilikimo pilimbi wa mashariki huwa na rangi inayofanana na majani yaliokauka.

Wao huliwa na ndege, nyoka na wa wadudu. Hapa Taita, hawa chura huliwa na ndege aina ya 'White-starred Robin' ambaye pia huwalisha vifaranga vyake.

kichula magala

Maelezo ya pembeni

Amietophrynus gutturalis







Todi wawili wakiogelea katika shimo limejaa maji ilikuchagua mahali pa kutagia mayai.

kiwandu

Dume hushikilia jike kwa nguvu ili kutunga mayai.

Huyu ndiye mmoja wa wale chura wanautabulika kwa urahisi na watu wa Taita. Wao hupatika kwa urahisi karibu na boma, mashamba, mashamaba makubwa na pia katika miisho ya misitu. Hii inaelezea jina lake ya Kitaita 'Kiwandu' kama chura wa watu. Huyu todi hupatikana katika sehemu kwanzia kule chini Mwatate hadi kule juu Vuria. Moja ya mambo ya kuvutia ni kutazama huyu mnyama akitokezea usiku karibu na mwangaza kushika wadudu wanaovutiwa na mwangaza. Hawa todi hupata mlo mkubwa usiku ule mchwa wanaruka. Todi wakubwa hula karibu kila kitu kinachotemebea na kinaweza toshea mdomo, ingawa chakula chao ni cha wadudu na konokono. Katika mashamba wao huwa wa faida sana kwani wao hula wadudu ambao huharibu mimea.

Vyura wa kiume huita mwaka mzima ingawa sauti zao huwa nyingi wakati wa mwanzo wa kipindi cha mvua.

Amietophrynus gutturalis (kuendelea)



Mayai yanatagwa mfano wa vijikamba kati ya mimea.

Sauti zao huwa kama kupasuliwa mbao (Rrrrrrrr Rrrrrrrrrr) na milio miingi pamoja husikika kutoka mbali. Todi ndume huita kutoka ndani mwa mahala pa kuzalia, katika vindibwi vya muda au vikubwa. Wale wa kike huvutiwa na milio ya ndume na hushikwa na wale ndume akipita. Chura wengi wa kiume hujaribu kushika jike moja na huwa mviringo wa wanyama. Mayai hutagwa kwa mikufu iliyo na maelfu ya mayai. Viluwiluwi vieusi huangua baada ya wiki moja na hurundikana pamoja. Wao huwa na sumu na hivyo hawawezi liwa na ndege na wanyama lakini huliwa na chura wa makucha na wadudu wa maji.

Baada ya miezi mbili, chura wadogo hutoka kwa maji na kuenda kwa sehemu zinazo zunguka maji. Wanaweza kuwa wengi mpaka wanakaa kama mkeka katika sehemu zingine na ni vingumu kukosa kuwankanyanga. Wengi huliwa na mahasimu hivyo kupunguza idadi katika miezi inayofuata wakati wanasambaa kwenye mazingira. Wakiwa wadogo ni rahisi kuwakanganya na *Arthroleptis xenodactyloides* (ukurasa 24) na

Chura huonekana karibu na nyumba, haswa kama kuna wingi wa chakula.

Viluwiluwi wanakaa weusi na wenye miili duara.

Phrynobatrachus cf. *scheffleri* (ukurasa 46). Sehemu za tambalale chini za Tsavo zinazozunguka Milima ya Taita pia huwa todi wawili wanaofanana; na wao ni todi wa Garmani na xeros. Todi wa Guttural hutambuliwa na msalaba wa kipekee kichwani kati ya macho. Huko Mlima Sagalla huyu todi husihi pamoja na todi wa Garmani ambaye uso wake hauna alama. Huyu todi huonekana kutoka milima ya Taita na sehemu zingine zilizoinuka Afrika mashariki kuteremka kusini hadi Durban nchini Afrika Kusini na magharibi hadi Angola.

Maelezo ya pembeni

Mertensophryne taitana





kiwandu kitini



Todi mbirikimo wawili wakielekea kwa kindibwi cha maji barabarani.

Huyu todi gumba wa Taita alitambuliwa mwanzo na wale waliopatikana huko Mlima Mbololo na Arhtu Loveridge miaka ya 1930, na akaipatia jina *taitana*. Toka wakati huo, huyu chura pia amepatikana katika sehemu za Tanzania, Congo, Zambia na Malawi. Hawa chura ni spesheli juu na tofauti dume huwa haziiti. Katika utafiti hivi majuzi huko Taita ilitambulika kuwa kama wakisumbuliwa wao hutoa sauti ndogo ya hofu (kama chura wengi), lakini hakuna sauti ya kuita iliyosikika. Lakini dume na jike hukusanyika kwa vidimbwi karibu na barabara Novemba, wiki kadhaa baada ya mvua ya vuli. Hawa chura wadogo (kimo cha milimita 25 hadi 35) na hukusanyika kila siku na mayai yakitagwa kwa kamba ndefu (kama mayai 300 kwa kila kamba).

Hawa viluwiluwi hunagua kutoka mayai haraka sana na kujifukia kwa

Mertensophryne taitana (kuendelea)



Kamba za mayai zikitagwa kwa maji ambapo huangua na kuwa vyura wadogo baada ya wiki mbili.



Vindimbwi kado ya barabara hukauka vikiacha viluwiluwi ambao huwa mlo wa wanyama wengine kama siafu.

matope kado ya kidimbwi ili kuia. Kila mmoja ako na kiungo spesheli juu ya kichwa ambayo husaidia kupumua juu ya upungufu wa hewa ya oksijeni. Hawa viluwiluwi hubadilika baada ya muda kama wiki mbili ambao ndio muda mfupi unaojulikana kwa chura yeyote. Baada ya ngono hawa todi hutoweka na kuonekana tena wakati wa kuzaana, Novemba. Baadhi ya hawa wanyama wamepatikana kwa mashamba ingawa ni mambo machache yanayo julikana kuwahusu mbali na mambo ya kuzaana. Wale wazima wako na tabia ya ajabu kutembea kwa miisho ya makucha na haijulikani kwa nini!

Wengi wa hawa chura wamepatikana Mbololo, na kuzaana kumeonekana kwa vindibwi barabarani. Kado na Mbololo hawa chura wamepatikana eneo la Macha, na hawapatikani kwa sehemu nyingi Taita.

Maelezo ya pembeni



Leptopelis concolor









Macho makubwa yanaonekana kwa mwangaza mdogo na vidole vipana vinavyosaidia kushikilia majani.

kichula mudi



Chura wa kiume ukaa juu ya mimea usiku na kutoa sauti ya kipekee.

Huyu chura anajulikana kutoka sehemu za chini za Taita. Ni kawaida kuona huyu churamiti mwenye rangi iliokwajuka kwa mashamba yenye maji. Yeye huketi kwa miti katika urefu kama mita moja na nusu juu, na dume huita kwanzia Oktoba hadi Aprili usiku vuguvugu, na wenye unyevu. Mwito wake unasehemu mbili; mwanzo ni sauti kubwa 'quack' ikifuatiwa na miunzi tatu inayodididimia. Mayai yanatagwa nje lakini karibu na maji, haswa juu ya mimea. Viluwiluwi wadogo kanza hukua ndani ya mayai na kuangua moja kwa moja ndani ya maji kama viluwiluwi wanao ogelea.

Wale wazima wana rangi ya hudhulungi na mfano wa shisha kwa mgongo (kama kichula magala). Wana macho makubwa yaliyokodolewa na kuonekana kwa kichwa. Wanayatumia kutafuta chakula katika mwangaza mdogo wa asubuhi na jioni.

Ingawa hawa chura wanafanana na churamiti wa glandikola (k.m. vidole vilivyo pana na vile wanaketi), wao hawana uhusiano. Huyu chura mwenye rangi iliyokwajuka ako kwa kundi moja na kichula magala.

Ptychadena mascareniensis







Chura wenye mikuja wanaweza patikana kwenye mitaro ya kunyunyizia maji mashamba na huruka ndani ya maji wakisumbuliwa.

kingele



Chura kigongo kiume ana mitungi ya masikio kubwa nyuma ya macho. Chini ya masikio iko mkato ambapo vifuko vya sauti hutokea wakati wa kuita.

Ingawa huyu chura ni mashuhuri yeye huonekana tu muda anaporuka toka kwa majani na kuingia majini na kuogelea mbali. Ukishika moja utaona yuko na mgongo ulio na mikujo na hivyo jina la hawa chura. Mchana hawa chura huwida katika miisho ya vindimbwi au mito yenye mwendo usio wa kasi, wakitafuta wadudu wadogo wa kula wanaoshikwa kwa kulamba na ulimi. Wakisumbuliwa, wao huruka mbele kuelekea ndani ya maji (kama yako karibu). Wao ni mahiri kwa kuruka na wanaweza kuruka mita kadhaa kwa kuruka mara moja.

Chura hawa huzaana Taita mwaka wote isipokuwa miezi kavu ya Juni hadi Septemba. Dume zina vifuko vya sauti ambavyo hufura kwa pande zote za kichwa na kutoa sauti ‘chrrr chrrr chrrr’ inayoweza sikika kwa mbali. Jike hutaga mayai ambayo huelea juu ya maji na kunagua na kuwa viluwiluwi vinavyo patikana hata kwa maji kado ya barabara.

Ptychadena mascareniensis (kuendelea)



Mayai yaonekana yakielea kwa muda wa wiki moja kabla ya viluwiluwi kuangua na kuingia majini.

Hawa viluwiluwi huchukua miezi miwili kuwa chura wadogo ambao huchukua miezi tisa kukomaa.

Huyu chura ni rafiki wa wakulima juu wao huwa wengi na hula wadudu waharibifu katika shamba. Yeye hufana na chura wa mikujo wa Anchieta (ukurasa 42) lakini hutofautiana na wa Taita kwa kuwa na mstari mweupe (rangi malai, kijani au hudhurungi) kwa mgongo hadi kwa kilele cha mapua. Dume ni wadogo kuliko jike na zaweza tambuliwa kwa chanja kwa pande zote mbili za kichwa mahali vifuko vya sauti huwekwa.

Hawa chura hupatikana kwa sehemu kubwa nje ya Taita kwa sehemu nyingi za kati na kusini mwa Afrika. Walakini, utafiti wa kijenetiki unaonyesha ni kikundi cha mkusanyiko wa vyura wengi na kwa hivyo jina laweza badilika

Viluwiluwi wa chura kigongo ukua miguu ya nyuma kwanza na upatikana kwa aina nyingi ya rangi.

baadaye. Hupatikana pia kwa visiwa vya Bahari Hindi na Madagascar. Hata kama huyu chura ameletwa na binadamu kwa hivi visiwa (hata Visiwa vya Mascarene pale alipotambuliwa kwanza) alifika kwa vingine kwa mimea iliyosombwa na mafuriko.

Maelezo ya pembeni

Ptychadena anchietae







Chura wa mikujo wa Anchieta wana umbo la miramba mitatu kati ya macho likipita hadi kwa mapua.



Chura kigongo wa Anchieta wanaweza patikana wakiwa wameketi pamoja pembeni ma maji usiku.

Huyu chura anakaa mahali sawa na chura wa Mascarene (ukurasa 38). Ingawa, huyu chura hupendelea kuishi kwa sehemu zilizo chini na yule wa Mascarene hupatikana kwa wingi huko milimani. Huyu chura hupenda kuruka na ataruka punde anaposumbuliwa. Kama hawezifika kwa maji kwa kuruka mara ya kwanza huruka tena ama kujificha chini kabisa kwa nyasi na kupitia katikati ya majani na kufanya kuwa vingumu kumshika.

Huyu chura anazaana wakakati wowote isipokuwa miezi iliyokauka (Juni hadi Septemba) na kwenye sehemu sawa na chura wa Mascarene; kwa vindibwi, na maji iliyosimama kado ya barabara. Wanatoa sauti kwa vifuko vya

Ptychadena anchietae (kuendelea)



Dume ziko na vifuko viwili za sauti zinozotokeza kwa chanja zilizo pande mbili za kichwa.

sauti kwa kila pande ya kichwa. Ile sauti inayotoka ni tofauti na inawezatabulika kwa kuwa ni kama 'wah wah wah'.

Huyu chura ameenea kwa Africa Mashariki, na wale wazima waweza tambuliwa kutoka kwa chura kigongo wa Mascarene kwa umbo la miraba mitatu kati ya macho hadi mapua. Huyu chura ni rafiki ya wakulima wa Taita juu hula wadudu wanao harribu mimea.

Vijiluwiluwi wa chura kigongo ukua dani ya mfuko maji ambao uelea majini.

Maelezo ya pembeni

Phrynobatrachus scheffleri







Chura mbilikimo wa Scheffler ni mdogo sana na hupitakana kado ya vijito mahali penye kivuli.

magala machi



Chura mbilikimo wa Scheffler ana matundu mawili yanayokaa herufi V kwa mgongo.

Hawa ni baadhi ya chura wadogo wanaopatikana Taita, wale wakubwa wana urefu wa milimita 22. Wanaweza patikana rahisi karibu na vijito na maji yanayododoka kwa nyasi, miti na misitu. Wao huruka haraka kwa matope au mchanga kando ya vijito wakishika inzi na wadudu wengine wanaotua hapo. Huyu chura anaweza kanganywa na yule wa *Arthroleptis xenodactyloides* (ukurasa 24), mbali na kuwa na alama ya msalaba mgongoni.

Dume huita kwenye sehemu zilizo jificha karibu na mahali wanapozaana na hutoa milio mifupi mifupi 'bzz bzz bzz'. Huyu chura hutaga mayai yameachana moja moja na huelea kwa vindimbwi kando ya vijito hasa vile vinavyotokea wakati wa mvua. Viluwiluwi hukua kwa hivi vindimbwi vidogo na kubadilika kuwa wadogo wanaoweza patikana kando mwa kijito.

Huyu chura hupatikana haswaa Afrika mashariki na kusini, lakini kunaaminika kuwa wanaweza kuwa wengi zaidi kado wanaotambuliwa.

Amietia angolensis









Dume zawezapatikana zimekaa kando ya mito kwenye sehemu zinazoonekana.

kichula moda



Hawa ni vyura wanene walio na miguu ya nyuma yenye nguvu ya kuogelea dhidi ya mkondo wa maji.

